# MISINGI YA USAWA WA JINSIA KATIKA KATIBA PENDEKEZWA

MTANDAO WA WANAWAKE NA KATIBA
WOMEN FUND TANZANIA

MTANDAO WA WANAWAKE NA KATIBA

# MISINGI YA USAWA WA JINSIA KATIKA KATIBA PENDEKEZWA

MTANDAO WA WANAWAKE NA KATIBA

WOMEN FUND TANZANIA

# YALIYOMO

Dibaji

Kwa nini kuwepo na dai la misingi ya usawa wa jinsia katika katiba

Dhana muhimu za masuala ya usawa wa jinsia

Hatua kuelekea katiba pendekezwa

Katiba pendekezwa na misingi ya usawa wa jinsia

Hitimisho

# DIBAJI

Kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania, wanawake kutoka nyanja mbalimbali, zikiwemo za kijamii, kiuchumi na kisiasa wali-ungana na kuunda MTANDAO WA WANAWAKE NA KATIBA TANZANIA. Muunganiko huu wa mashirika/asasi yaliyozidi 50 yasiyo kuwa ya kiserekali na watetezi binafsi watetezi wa haki za binadamu na hususani za wanawake na watoto wa kike una lengo la kuhakikisha kuwa Katiba mpya inayoandaliwa inajengewa misingi imara yenye mrengo wa jinsia.

Katika mchakato mzima wa kushinikiza misingi ya usawa wa jinsia katika Katiba Pendekezwa,Wanawake na Katiba Tanzania, unatambua juhudi kubwa zilizofanywa na watu mablimbali, wakiwemo WanaMtandao, Mashirika na Wanawake Binafsi waliojitolea kwa hali na mali, wabunge wa Bunge Maalum la Katiba walioshriki katika michakato ya Mtandao huu, na wafadhili rafiki waliokuwa wanatupa moyo na kutushauri hapa na pale. Mtandao unatambua pia mchango wa vyombo vya habari katika kujengea umma ufahamu kuhusu mchakato wa Katiba na hasa kuhusu kwa nini ni muhimu Katiba Mpya izangatie misingi ya usawa wa jinsia iliyo imara.

# KWA NINI KUWEPO NA DAI LA MISINGI YA USAWA WA JINSIA KATIKA KATIBA?

**Uwepo wa dai la misingi imara ya usawa wa jinsia katika Katiba Mpya, inatokana na ukweli kwamba** historia ya mapambano dhidi ya mifumo kandamizi, wanawake wamekuwa wakishiriki bega kwa bega na wanaume. Hata hivyo mara zote, ushindi unapopatikana, wanawake wamekuwa wakisukumwa pembezoni kwa madai kwamba hawana uwezo wa kushika hatamu za utawala. Kwa mfano, wakati wa kupigania uhuru, wanawake walikuwa mstari wa mbele kwenye harakati zote lakini uhuru ulipopatikana wanawake hawakushirikishwa kikamilifu kwenye ngazi za maamuzi hadi walipoanza kudai haki hiyo. Historia hii ni funzo ambapo kulipotokea fursa ya mchakato wa kutayarisha Katiba mpya ilionekana ni vyema wanawake kuunganisha nguvu chini ya Mitandao mbalimbali ukiwemo ule wa Mtandao wa Wanawake na Katiba Tanzania, wakiwa na lengo la kushirki na kushinikiza katika ngazi mbalimbali za mchakato wa kurekebisha Katiba kwa sauti moja yenye nguvu ili Katiba Mpya izingatie, iheshimu na kulinda misingi ya usawa wa jinsia katika Sehemu na Ibara zote kuu.



# DHANA MUHIMU ZA MASUALA YA USAWA WA JINSIA

Ili kufahamu kile kinachopiganiwa na Mtandao wa Wanawake Tanzania katika Katiba Mpya, kuna dhana muhimu zinazopaswa kueleweka kwa kina. Dhana hizi zipo nyingi lakini katika Jedwali hili zimetajwa chache:

**Jinsi:** Ni dhana inayotumika katika kuelezea tofauti za kimaumbile kati ya mwanamke na mwanaume.

Kwa kawaida, binadamu huzaliwa na jinsi ya kike au kiume. Jinsi hizi ni tofauti ya kibaologia na hazihusiana na nani kati ya mwanamke au mwanaume ni wa hali ya juu zaidi ya mwenzake.

**Jinsia:** Ni dhana ambayo hutumika katika kuelezea mahusiano ya kijamii yaliyojengeka kati ya mwanaume na mwanamke. Dhana hii hutumika kuelezea tafsiri ya jamii kuhusu maana ya kuwa mwanamke au mwanaume, ikiwa inatoa utofauti katika thamani ya utu wao, stahili na haki zao pamoja na nafasi zao kama vile: wajibu au kazi, madaraka, maamuzi, umilki wa rasilimali n.k. Hivyo basi, dhana hii mara nyingi hutumika katika kutoa tafsiri ambayo inaelezea mahusiano yanayooundwa na jamii, na ambayo huwa nje ya tofauti za kibaolojia kati yao. Tafsri hii ya kijamii ambayo mara nyingi huimarishwa na mifumo ya kidini, kielimu na kisera/bajeti, inatoa tafsiri au inaashiria kumbebesha mwanamke wajibu mkubwa na kumyima haki sawa na hasa usawa wa kufikia, kufaidi huduma za kijamii, kumiliki raslimali za nchi, kufaidi matunda ya jasho lao pamoja na ushiriki ulio imara katika maamuzi yanayogusa maisha ya jamii kutoka ngazi ya familia, kitaifa na kimataifa, na hata wakati mwingine kuondoa utu na thamani ya maisha yao iliyo hafifu. Kwa kuwa mahusiano haya yasiyolingana kijinsia yamejengwa na wanajamii (wakiume na wakike) yanaweza kubadlishwa na ya kaleta uswa wa kijisia weneye tija katika jamii.

**Masuala ya Udhalilishaji Kijinsia:** Hutokea pale ambapo tafsiri za jamii kuhusu haki, wajibu na majukumu inaashiria kujenga tabaka au mapengo kati ya mwanamke na mwanaumekatika ngazi mbalimbali. Mapengo haya ya kijinsia hupelekea kuwepo kwa: *Mapengo ya Jinsia, Ubaguzi wa Jinsia na Ukandamizaji wa wanawake kijinsia.*

**Mapengo ya Kijinsia:** Hii hutokea pale ambapo majukumu ya kijinsia huleta urari usio sawia katika mgao wa uzito wa kazi na ule wa mapato. Kwa ufupi, mapengo ya kijinsia hutokea pale ambapo kumekosekana haki (social justice) kati ya mwanamke na mwanaume na hivyo kuna...

**Ubaguzi wa Kijinsia. Kwa mfano, ubaguzi huu unaweza kuwa katika** utoaji wa huduma tofauti, au haki tofauti ambazo hazizingatii misingi imara, ya ujenzi wa uaswa kati ya wanawake na wanaume. Katika jamii nyingi nchini, hali hii ya ubaguzi wa kijinsia, hujitokeza kwa mfano katika ubaguzi wa muundo wa kijinsia dhidi ya wanawake kuhusiana na mapato, ufikiaji wa huduma na raslima-li na kushiriki katika maamuzi nyeti yanayohusu maisha yao na ya kijamii.

**Usawa wa Jinsia:** Hii ni hali ya kutokuwa na ubaguzi kwa misingi ya jinsi ya mtu katika nyanja mbalimbali zikiwemo mgao wa raslimali au mapato au katika kufikia huduma mbali mbali za jamii. Kuna usawa wa jinsia wa aina mbili, japokuwa aina zote hizi ni muhimu na hujengeana katika kuleta tija na mabadilko katika maisha ya wanawake (na wanaume) wanaodhalilishawa na kukandamizwa na mifumo inayowasogeza pembezoni. Kwa mfano, kuna usawa wa jinsia unaopelekea zaidi katika kuwepo kwa fursa sawa au usawa unaopelekea wanawake katika kupigania fursa sawa katika ufikiaji wa elimu, afya, umiliki mali na mengineyo. Japokuwa usawa wa namna hii ni muhimu, mara nyingi hupelekea katika uaswa wa kuziba mapengo, na unaongalia namba za ushiriki kati ya wanawake na wanaume katika nafasi mbalimbali. Usawa huu hujulikana kama usawa wa kufikia fursa zinazolingana (Gender Equity). Hata hivyo, mara nyingine usawa huu hauleti mabadiliko katika mifumo kandamizi.

Aina ya pili ya usawa wa jinsia ni ule unaopelekea katika kufumuliwa kwa mifumo kandamizi ili kujenga mazingira rafiki na yanayomletea mabadilko yennye tija anayekandamizwa (Gender Equality). Usawa huu wa jinsia ni muhimu katika kujenga mazingira ya usawa katika ngzai mbalimbali (Gender equality) hupimika kwa kuwepo kwa misingi au mihimili mikuu ya kikatiba yenye kuleta usawa wa jinsia, pia hupimika kwa uwepo wa sheria zinazotoa na kulinda haki za wanawake na wanaume kwa usawa unaoleta tija, miundo, sera na bajeti chanya za serikali kuhusu usawa wa jinsia katika ngazi mbalimbali.

# HATUA KUELEKEA KATIBA PENDEKEZWA

Katika kushinikza madai ya Mtandao wa Wanawake na Katiba katika ili Katiba mpya, kulikuwepo na hatua kadhaa zilizojitokeza na kutoa fursa kwa WanaMtandao:

## 1. Uchambuzi wa Masuala ya Kudai

**Hatua hii ilitoa fursa kwa WanaMtandao** kutambua mapungufu ya kijinsia yaliyopo katika kila sekta na kuweza kuyaainisha pamoja kufikia muafaka wa masuala/misingi muhimu ya kuingizwa kwenye Katiba Mpya. Hatua hii pia ilitoa fursa, kwa Mtandao wa Wanawake na Katiba kutafakari kwa pamoja na kwa kina, juu ya masuala ya jinsia au misingi itakayopelekea kupatikana kwa Katiba mpya yenye mrengo imara kwenye eneo zima la kuleta usawa wa jinsia. Mikutano kadhaa iliyohusisha wanawake wa ngazi mbalimbali iliandaliwa na ulinganifu wa Katiba za Afrika na kimataifa zilichambuliwa ili kuona ni ipi (au sehemu ipi ya Katiba hizi) inaendana na hali ya Tanzania, hususan katika kujenga na kulinda haki za mwanamke na mtoto wa kike. Masuala yaliyojitokeza yalikuwa mengi kwa vile zilikuwa Asasi nyingi, na kila mojawapo ikiwa na suala lake la kipa umbele kwenye Katiba. Kwa njia ya majadiliano na hatimaye, kwa kuzingatia kwamba Katiba ni sheria mama inayotokeza misingi mikuu ya kulinda haki za kiraia, Mtandao ulikubaliana na masuala au madai kumi na mbili (12) ya kuingizwa kwenye Katiba Mpya inayoandaliwa.

| MADAI 12 | |
|---|---|
| Madai makuu ya Wanawanake na Katiba yalikuwa kwamba, Katiba izingatie: | |
| **1. Haki za Wanawake zibainishwe kwenye Katiba Mpya:** | Haki za msingi za wanawake zibainishwe katika Tamko la Msingi wa Haki za Binadamu (Bill of Rights) ili wanawake waweze kupata haki sawa za uraia, siasa na uchumi na ustawi wa jamii zitakazolindwa kikatiba. |
| **2. Sheria Kandamizi zibatilishwe:** | Katiba Mpya ibatilishe sheria zote za ubaguzi wa jinsia, ikiwa ni pamoja na kukataza mwendelezo wa tabia, taratibu na mila zenye kubagua na kudhalilisha wanawake na watoto wa kike. |
| **3. Utu wa mwanamke ulindwe:** | Katiba iweke bayana misingi itakayolinda utu wa mwanamke ikiwa ni pamoja na kulinda wanawake dhidi ya vitendo vya ukatili dhidi yao kama: *ukatili wakijinsia, ubakaji ndani na nje ya ndoa, ukeketwaji wa watoto wa kike, ndoa za utoto, na vitendo vingine vya ukatili dhidi ya wanawake na watoto wa kike.* |
| **4. Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa kuhusu Haki za Wanawake:** | Katiba mpya iwajibishe serikali kutekeleza mikataba yote iliyoridhia kuhusu haki za wanawake. Mikataba hii itambulike kuwa ni sheria za nchi ili kuepusha ucheleweshaji wa kutafsri au kuruhusu tafsiri zinazokinzana na misingi ya mikataba husika. |

| | |
|---|---|
| **5. Haki sawa katika nafasi za uongozi: Haki za Wanawake:** | Katiba mpya ibainishe misingi itakayoweka usawa wa kijinsia katika ngazi zote za uongozi pamoja na maamuzi.. Serikali iwajibishwe kuchukua hatua za kisera na sheria ili kuhakikisha wanawake wana-shiriki kwa uwiano sawa katika nyanja zote za uongozi pamoja na a uongozi wa mihimili mikuu mitatu ya utawala (serikali, Bunge na mahakama) kwa kuzingatia mkataba wa AU (50/50) unafikiwa mapema/ haraka. |
| **6. Haki za Watoto wa Kike:** | Katiba Mpya ieleze bayana umri wa mtoto ili imlinde moto wa kike dhidi ya ndoa za utotoni na iweke msingi utakaolinda haki za mtoto wa kike katika kufikia na kufaidi huduma za jamii ikiwa ni pamoja na elimu yenye kuwawezesha kudai, kutetea na kulinda haki zao; kumlimda mtoto wa kike dhidi ya ukatili wa kijinsia. |
| **7. Haki ya kufikia, kutumia, kunufaika na kumiliki rasilimali ya nchi:** | Kwa kuzingatia kwamba rasilimali ya nchi yetu ni ya kila Mtanzania (me na Ke) katiba iweke bayana kwamba mwanamke wa Kitanzania anazo haki sawa za kufikia, kutumia, kumiliki na kufaidi rasilimali za nchi yetu ikiwa ni pamoja na ardhi, madini, na vitu vyote vilvyoko nchi kavu na majini. |
| **8. Haki ya Uzazi Salama:** | Katiba mpya ihakikishe afya ya uzazi inalindwa kikatiba ili kumhakik-ishia mwanamke haki ya uzazi salama. Serikali iwajibishwe kuwekeza katika afya ya uzazi kwakwa jumla pamoja na mpango wa uzazi kutambua mzigo mkubwa anaobebeshwa mwanamke katika kuen-deleza kizazi cha Tanzania, na kuashiria kuweka rehani haki yao ya msingi ya kuishi, kutokana na changamoto wanazokumbana nazo wakati wakitimiza jukumu hili la uzazi. |
| **9. Haki za Wanawake wenye Ulemavu:** | Katiba mpya iainishe haki za wanawake wenye ulemavu kwa kutam-bua kwamba kundi hili huathirika mara dufu na mfumo dume. Katiba mpya iiwajibishe serikali kuchukua hatua za kisera na kisheria ili kulinda wanawake wenye ulemavu dhidi ya vitendo vya ukatili, naku-fikia huduma za msingi za kukimu maisha kama vile huduma za afya, elimu, hifadhi ya jamii, kutokubaguliwa katika ajira. |
| **10. Haki ya kufikia na kufaidi huduma za msingi:** | Katiba ibainishe haki sawa kwa wanawake za kufikia huduma za msingi ikiwa ni pamoja na afya, elimu, maji, huduma za hifadhi ya jamii. |
| **11. Kuwepo kwa Tume ya Usawa wa Kijinsia:** | Katiba Mpya iwajibishe bunge kuunda chombo kitakachosimamia utekelezwaji wa haki zinazodaiwa kama chombo kimoja cha uwajibi-kaji kuhusiana na masuala ya uswawa wa kijinsia. |
| **12. Mahakama ya Familia:** | Katiba mpya iweke msingi wa kuwepo sheria ya uundaji wa mahakama za familia ili kukufanikisha upatikanaji wa haki kwa wakati unaofaa. |

## 2. Kuelimisha Jamii Kuhusu Madai

Kampeni ya kitaifa ilifanyika kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu msingi na madai ya wanawake. Mtandao wa Katiba Tanzania ulipanga na kufanyika mfululizo wa mikutano, semina na vikao katika ngazi mbalimbali nchini. Wanamtandao katika maeneo yao ya utendaji walijishughulisha kuielimisha jamii na kutoa maelezo kuhusu msingi wa madai ya wanawake. Mikutano na Wahariri na wanahabari ilifanyika kwa nyakati tofauti katika kufahamisha hoja za wanawake na kuhamasisha matumizi ya programu za vyombo vya habari, kubeba ujumbe wa madai ya wanawake ili yafahamike na kujadiliwa na umma mkubwa wa Watanzania.

## 3. Kuwasilisha kwa Tume ya Katiba

Mtandao uliwasilisha madai yake 12 kwa Tume ya Katiba. Hii ilikuwa nafasi nzuri kwa wanaMtandao kwa nafasi zao na katika asasi zao na pia Mtandao kwa ujumla. Tume ya Katiba iliyachukua madai haya na kuonyesha kufurahishwa na jinsi ambavyo Mtandao uliweka bayana madai hayo. Tume ilishauri Mtandao ujitahidi katika kuelimisha wananchi, wanawake kwa wanaume, wayaelewe madai haya na kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kuandaa Katiba Mpya.

## 4. Uchambuzi wa Rasimu

Zoezi kubwa baada ya kutoka kwa Rasimu ya kwanza ya Katiba, ilikuwa ni kuichambua na kuitathmini ili kuona kama yale yaliyo-ingizwa na ambayo yaliacha. Baada ya hapo, mapendekezo ya Mtandao yaliwasilishwa tena kwa Tume ya Katiba.

## 5. Kuelimisha na Kushawishi Wabunge wa Bunge Maalum la Katiba

Kazi ya kuhamasisha, kuelimisha na kupigania hoja za wanawake ziliendelea wakati wa Bunge Maalum la Katiba. Wakati huu ulikuwa ni mahsusi kwa ushawawishi wa wabunge kwa kupitia mikutano ya ana kwa ana, mikutano ya pamoja na semina. Hizi ziiendelea hata wakati Bunge Maalum la Katiba lilipoahirisha kikao kwa miezi kadhaa.






Hatua na juhudi zote hizo zilichukuliwa na Mtandao wa Wanawake na Katiba zilikuwa kwanza kujenga nguvu za pamoja kati ya makundi mbalimbali ya wanawake nchini na kutumia nguvu hiyo kutokeza sauti au madai yao huku wakishinikiza kupitishwa kwa masuala au madai 12 yaingizwe katika Katiba mpya.

# KATIBA PENDEKEZWA NA MISINGI YA USAWA WA JINSIA

Kwa kiasi kikubwa, Katiba inayopendekezwa imezingatia masuala mengi yaliyopendekezwa na Mtandao wa Wanawake na Katiba Tanzania. Kijitabu hiki kinawasilisha misingi au mihimili mikuu ya Kikatiba iliyojitokeza katika Sura na Ibara za Katiba Pendekezwa:

| IBARA | ISEMAVYO IBARA HII KATIKA KULETEA MISINGI YA KIKATIBA KWA MRENGO WA USAWA WA JINSIA | ILIVYOKIDHI MAPENDEKEZO YA MTANDAO WA WANAWAKE WA KATIBA TANZANIA |
|---|---|---|
| UTANGULIZI | **Aya ya Kwanza:** KWA KUWA, sisi wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) tumeamua rasmi na kwa dhati kujenga katika nchi yetu jamii inayoheshimu na kuzingatia misingi ya **utu, uhuru, haki, usawa, udugu,** amani, umoja na mshikamano katika nyanja zote za maisha yetu.<br><br>**Aya ya sita:** Na kwa kuzingatia, urithi ulioachwa na Waasisi wa taifa letu wa kujenga nchi yenye umoja wa watu wake ambao hawabaguani kwa misingi ya **ukabila, dini, rangi, jinsi, ulemavu au ubaguzi wa aina nyingine yoyote** | Katiba Pendekezwa imekiri dhamira ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) wa kujenga nchi yenye misingi inayoongozwa na utu, uhuru, haki, usawa n.k. Kwa wanawake wengi katika nchi hii, kuwepo kwa misingi hii ni muhimu wa kuondokana na uonevu na udhalilishaji unaotokea kwenye ngazi mbalimbali za maisha yao. Misingi hii ya kuletea usawa wa jinsia, inapewa nguvu zaidi katika Aya ya sita ambapo ubaguzi wa aina yoyote unapingwa ikiwa ni pamoja na ubaguzi wa jinsia.<br><br>**HII INA MAANA MSINGI WA USAWA WA JINSIA UMEBAINISHWA KAMA MSINGI MMOJAWAPO WA UTAWALA BORA NCHINI** |
| SURA YA 1: JINA, MIPAKA, ALAMA, LUGHA NA TUNU ZA TAIFA | **Ibara ya 6(2):** Misingi ya utawala bora katika JMT itajumuisha **(g)** Usawa wa jinsia<br><br>**Ibara 8(2):** Kwa madhumuni ya masharti ya **Ibara ndogo ya (1);** serikali na vyombo vyake vinawajibika kuelekeza sera, sheria na shughuli zake zote kwa lengo la kuhakikisha kwamba **(a)** utu, heshima na haki za binadamu zinalindwa, zinathaminiwa, zinahifadhiwa kwa kuzingatia mila na desturi za Watanzania na mikataba ya kimataifa iliyoridhiwa na JMT **(e)** maendeleo ya uchumi wa Taifa yanapangwa na kukuzwa kwa ulinganifu na kwa namna ambayo inawanufaisha wananchi wote; **(g)** kunakuwepo fursa a haki zilizo sawa kwa wananchi wote, wanawake na wanaume, bila kujali rangi, kabila, nasaba, ulemavu, itikadi, dini au hali ya mtu; **(h)** aina zote za dhuluma, vitisho, ubaguzi, ukatili, udhalilishaji, unyanyasaji, rushwa, uonevu au upendeleo zinaondolewa nchini | Msingi wa Kikatiba unaolenga kuimarisha utawala unaozingatia usawa wa jinsia ni muhimu katika kujenga demokrasia ya kweli nchini. Kuingizwa kwa nguzo hii ya utawala bora ni **FANIKIO** kubwa katika harakati za kuendeleza wanawake nchini.<br><br>Katiba Pendekezwa imetambua ulinzi wa utu, heshima na haki za binadamu. Aidha inataka dhana hizi zidumishwe kwa kuzingatia mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa. Kwa kuitambua mikataba ya kimataifa na kikanda kutasaidia kuondoa ubaguzi, unyanyasaji na matumizi mabaya ya mila potofu.<br><br>**KWA TAIFA HILI KUTAMBUA UMUHIMU WA MSINGI WA HAKI YA KIKATIBA INAYOLINDA UTU, NA HESHIMA YA WANWAKE WA NCHI HII, NI FANIKIO KUBWA, HASWA IKIZINGATIWA KUWA (WAKATI MWINGINE) MIFUMO MBALI MBALI, IKIWEMO YA KIUTAMADUNI INARUHUSU SHERIA ZA KIMILA AMBAZO HUPELEKEA ULINZI WA UTU, HESHIMA NA HAKI ZA BINADAMU KUTOZINGATIWA KWA KIKAMILIFU** |

| | | |
|---|---|---|
| | **Ibara ya (9)(4):** Sheria yoyote, mila, desturi au uamuzi wowote wa chombo cha dola au ofisa wa Serikali ni sharti ufuate na kuzingatia masharti yaliyomo kwenye Katiba hii na kwamba sheria, mila, desturi au uamuzi wowote ambao hautawiana au kwenda sambamba na masharti ya Katiba hii utakuwa batili | katiba pendekezwa inatamka wazi kuwa **"katiba ndiyo sheria kuu ya nchi kwa masharti yote yaliyopo kwenye katiba hii na kwamba kwa masharti yote yaliyopo kwenye katiba hii na kwamba masharti ya sheria yeyote itakayo-tungwa na kutofuatiana na masharti ya katiba hii yatakuwa batili na yatatenguliwa"** |
| **SURA YA 2: MALENGO, MWELEKEO WA SHUGHULI ZA SERIKALI NA SERA ZA TAIFA** | **Ibara ya 11(1):** Lengo la Katiba ni kulinda, kuimairisha na kudumisha haki, usawa, udugu, amani, umoja na utangamano wa wananci wa Jamuhiri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuzingatia ustawi wa wananchi na kujenga Taifa huru lenye demokrasia, utawala bora, maendeleo endelevu na kujitegemea | Katiba Pendekezwa inakiri kwamba lengo kuu la Katiba Mpya ni **KULINDA, KUIMARISHA NA KUDUMISHA HAKI, USAWA, UDUGU, AMANI, NA UTENGAMANO WA WANANCHI** |
| | **Ibara ya 12(2):** Katika kuhakikisha utekelezaji wa lengo la kudumisha demokra-sia na kuondoa ubaguzi wa aina zote, serikali itachukua hatua zinazofaa ili, **(a)** kuhakikisha kuwa inazuia na kuondoa dhuluma, vitisho, ubaguzi, unyanyasaji, rushwa, uonevu n aupendeleo miongoni mwa wananchi kwa misingi ya itikadi, asili ya mtu, sehemu anayotoka, nasaba, kabila, jinsi, dini au imani yake | Ibara hii ya Katiba Pendekezwa inazuia na kuondoa dhuluma, rushwa, ubaguzi wa kidini, jinsi n.k. Hii inamaanisha kuwa msingi wa usawa wa jinsia umezin-gatiwa na NIA ni kuondoa ubaguzi, unyanyasaji na uonevu. Hili ni fanikio kwa kuwa ubaguzi ukiwemo wa kisiasa ume-fanywa sehemu muhimu ya malengo ya kisiasa. |
| | Lengo la Taifa la Kiuchumi; **Ibara ya 13 (2)(g)** kuhakikisha kwamba shughuli za Serikali zinatekelezwa kwa njia ambazo utajiri wa taifa unatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa kuweka mazingira yatakayochochea maendeleo linganifu na kuwawezesha wananchi kuondokana na umaskini; | Huu ni msingi muhimu sana wa kikatiba kwa maisha ya wanawake, hasa kwa walio na hali duni, kwa kuwa ulinzi wa rasilimali za nchi na jinsi zitakavyogawanywa kwenye hali ya ulinganifu zaidi umewekwa kikatiba. Msingi huu unategemewa ujengee katika kuletea wananchi maskini, wengi wao wakiwa wanawake wasio na hali nafuu ya maisha |
| | Lengo la taifa kijamii; **Ibara ya 14(2)(b)** Kuhakikisha kwamba Serikali na vyombo vyake vyote vya um-ma vinatoa nafasi na fursa sawa kwa raia wote, bila ubaguzi; **14(2)(d)** kuwezesha upatikanaji na utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za mawakili; **14(2)(f)** kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora ya afya kwa watu wote ikiwa ni pamoja na afya ya uzazi salama | Misingi iliyojengewa kwenye Ibara hii ya Katiba Pendekezwa, inatoa mwanya mkubwa wa raia waliowekwa pembezoni na mifumo mbalimbali, ikiwemo mifumo kandamizi ya mifumo dume au ya kitabaka kufaidi zaidi katika kupata huduma za misingi kama afya ya uzazi bila ya ubaguzi. Kwa mfano, utoaji wa huduma wa sheria utawasaidia sana wanawake wa vijijini na wale maskini wa mjini kufikia suluhisho za kisheria kwa urahisi na wenye kuleta tija kwenye maisha yao |

| | | |
|---|---|---|
| | **Ibara ya 19(1):** Malengo ya Taifa yaliyoainishwa katika Katiba hii yatakuwa ni mwongozo kwa serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wananchi katika matumizi au kutafsiri masharti ya Katiba hii au sheria nyingine yoyote au katika utekelezaji wa maamuzi ya kisera kwa madhumuni ya kujenga jamii iliyo bora, huru na makini<br><br>**Ibara ya 19(2):** Serikali ya Jamhuri ya Muungamo wa Tanzania itawasilisha bungeni mara moja kwa mwaka, taarifa ya hatua zlizozichukua katika utekelezaji wa malengo ya Taifa | Malengo ya taifa ni muhimu sana katika kuongoza utekelezaji wa kitaifa katika ngazi mbalimbali, hivyo kujengewa msingi wa kuhakikisha serikali inatambua hili na kwamba itayatolea taarifa bungeni ni hatua muhimu ya kuhakikiksha malengo haya yanaleta tija kwa wananchi, wakiwemo wanawake. |
| **SURA YA 3: ARDHI, MALI ASILI NA MAZINGIRA** | **Ibara ya 23(2):** Ardhi yote itamilikiwa, itatumiwa na itasimamiwa kama itakavyoainishwa na sheria zinatazotungwa na Bunge au Baraza la wawakilishi kwa kadri itakavyokuwa, kwa kuzingatia misingi ifuatayo **(d)**: kila mwanamke atakuwa na haki ya kupata, kumiliki, kutumia, kuendeleza na kusimamia ardhi kwa masharti yale yale kama ilivyo kwa wanaume | Kwa mara ya kwanza katika historia ya Katiba za Tanzania, Ardhi ambayo ni raslimali muhimu sana katka nchi ime-pewa uzito stahiki kwa kupewa sura yake katika rasimu, tofauti na Katiba nyingine zote zilizotangulia ambako ardhi ilitajwa juu juu tu, au kutotajwa kabisa. Zaidi ya hapo, kwa mara ya kwanza Sheria Mama inatoa haki ya umilikaji ardhi kwa misingi iliyo imara zaidi kwa wanawake na hivyo kuondokana na sheria za kijadi ambazo zilikuwa zinakwenda sambamba na sheria za nchi katika Katiba ya mwaka 1977 |
| **SURA YA 4: MAADILI & MIIKO YA UONGOZI NA UTUMISHI WA UMMA** | **Ibara ya 28(2):** Mtu mwenye dhamana ya uongozi wa umma atazingatia mambyo yafuatayo **(a)** anapokuwa anafanya maamuzi ya uteuzi atahakikisha kwamba anafanya uteuzi bila ubaguzi ila kwa kuzingatia uwezo, sifa na mwenendo unaofaa **(b)** anapokuwa anafanya uamuzi wowote katika jambo lolote katika madaraka anayopewa kiongozi wa umma atahakikisha uamuzi wake hautokani na udugu, ukabila, udini, rushwa au **ubaguzi wa aina yoyote** | Ingawa kuzingatiwa kwamsingi wa usawa wa jinsia hakuwekwa bayana katika Ibara hii, ubaguzi wa aina yoyote utakakuwa kinyume cha Katiba. Hii in maana kuwa usawa wa jinsia utazingatiwa kama sehemu ya maadili na miiko ya uongozi na utumishi wa umma. |
| **SURA YA 5: HAKI ZA BINADAMU, WAJIBU WA RAIA, JAMII NA MAMLAKA YA NCHI** | **Ibara 51(1):** Kila mtu ana haki ya kupata huduma ya afya na maji safi<br><br>**Ibara 52(1):** Kila mtu ana haki ya kupata elimu bora ya msingi inayomtayari-sha kikamilifu kuendelea na elimu ya ngazi inayofuatia au kuweka msingi wa kuanza kujitegemea<br><br>**Ibara 53 (1):** Kila mtoto ana haki ya **(b)** kutoa mawazo, kusikilizwa na kulindwa dhidi ya uonevu, ukatili, udhalilishaji, utumikishwaji na mila potofu na **(3):** Kwa madhumuni ya ibara hii "mtoto" maana yake ni mtu mwenye umri chini ya miaka kumi na nane. | **Ibara 32-67** za sura, hii zimetaja haki mbalibali za binadamu. Mathalani, hakı kuish, uhu-ru, utu, usaca wa binadamu, haki ya kutobaguliwa, kupata haki sawa mbele ya sheria, marufuku ya ubaguzi ila Katiba inatambua ubaguzi kwa mrengo wa kuyapatia makundi maalum nafasi mbalimbali au stahiki au fursa sawa.<br><br>Jambo hili la Katiba Pendekezwa kuingiza Haki za binadamu na hususani |

| | | |
|---|---|---|
| | **Ibara ya 55:** Haki za watu wenye ulemavu zikiwemo **(c)** Kuwekewa miundombinu na mazingira yanayofaa kumwezesha kwenda anapotaka, kutumia vyombo vya usafiri na kupata habari; **(d)** lugha ya alama, alama mguso, maandishi ya nukta nundu, maandishi yaliyokuzwa au njia nyingine zinazofaa; kupata huduma bora za afya, uzazi salama, marekebisho na utengemano | kuanisha haki za mwanamke katika Iba-ra hizi ni jambo la kihistoria. Kwa mfano, kwa mara ya kwanza suala la haki ya maki limeingizwa kwenye Katiba. Ukosefu wa maji ni tatizo kubwa kwa wananchi maskini na hasa kwa wanawake.<br><br>Ingawa tungependa kuona kiwango cha haki ya Elimu, kuwa zaidi ya kidato cha Nne, huu ni msingi ulio na tija kwa watoto, hususan kwa watotot wa kike. Msingi huu utatoa fursa na kumpatia nafasi mtoto wa kike kupata elimu na kumuepusha asiozwe akiwa bado mtoto. Ni dhahiri kuwa, watoto wa kike wakipata fursa za kusoma mpaka Kidato cha Nne (na zaidi) atakuwa amefikisha miaka 18 na hivyo kuweza kufanya maamuzi.<br><br>Pia kwa mara ya kwanza kikatiba, umri umetamkwa bayana. Kwa kuzingatia ukuu wa Katiba, sheria zinazoruhusu mtoto wa kike kuolewa kabla ya miaka 18, sasa zitabadilishwa na hivyo kufuta ndoa za utotoni.nchini.<br><br>**Haki za watu wenye ulemavu** zimeainishwa katika malengo ya Katiba Pendekezwa. Pia imetambua mawasiliano mbadala husasani lugha ya alama, lugha ya alama mguso, maandishi yaliyokuzwa, pamoja na nukta nundu kwamba zitakuwa lugha rasmi za mawasiliano. Vilevile ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu umepigwa marufuku.<br><br>**Hili ni FANIKIO** zuri, wanawake hasa wale wanaoishi na ulemavu kwani sasa wana haki sawa kikatiba na endapo watabaguliwa au haki zao kupokonywa kwa namna moja au nyingine wanaweza kuzidai mahakamani.<br><br>**Haki za watu wenye ulemavu** zimetambuliwa na katika ibara ya 56 ni haki za makundi madogo madogo katika jamii.<br><br>**Haki za wanawake** zimeboreshwa na kuingiza haki ya ku-pata huduma bora ya afya ikiwemo afya ya uzazi salama na pia haki ya kumiliki ardhi, haki sawa katika ajira pamoja na haki ya kulindwa ajira ya mwanamke wakati wa ujauzito na anapojifungua.<br><br>**Haki za wazee;** Ibara hii imeboreshwa kwa kuongezwa vipengele vya miundo mbinu, kupata huduma za matibabu, kulindwa dhidi ya unyonyaji, ukatili, mateso na mauaji) Hii itakomesha mauaji ya vikongwe yanayo-tokea mara kwa mara. |
| | **Ibara 57:** Haki za wanawake ikiwemo **(a)** Kuheshimiwa, kuthaminiwa na kutambuliwa utu wake; **(b)** Kulindwa dhidi ya ubaguzi, udhalilishaji, dhuluma, unyanyasaji, ukatili wa kijisia na mila potofu; **(c)** Kushiriki bila ubaguzi katika uchaguzi na ngazi zote za mamuzi; **(d)** Kulindwa ajira yake wakati wa uja uzito na pale anapojifungua; **(e)** Kupata huduma bora ya afya ikiwemo afya ya uzazi salama; **(f)** Kumiliki mali | |
| | **Ibara 58:** Haki za wazee ikiwemo **(c)** Kupata huduma za matibabu **(d)** Kulindwa dhidi ya unyonyaji, vitendo vya ukatili ikiwemo mateso na mauaji **(f)** Kupata mahitaji ya msingi kutoka kwenye familia yake, jamii na inapobidi mamlaka ya nchi | |

## USIMAMIZI WA HAKI ZA BINADAMU

Katiba Pendekezwa imeweka utaratibu wa namna ya kusimamia haki za binadamu zilizotajwa hapo juu. Utaratibu huu umeanishwa katika ibara ya 65 na hata namna ya kudai haki hizo mahakamani. Imetamkwa kuwa:

**65-(1)** Katika kutafsiri masharti ya Sura hii ya Haki za Binadamu, Mahakama au chombo kingine chochote cha kufanya uamuzi kitazingatia mambo yafuatayo:
- **(a)** sheria za kimataifa na haki za binadamu; na
- **(b)** haki za jamii na maslahi ya jamii kwa ujumla.

**(2)** Mtu anayeamini kuwa masharti yaliyomo katika Sura hii yamekiukwa au yanaelekea kukiukwa na mamlaka, chombo cha uamuzi, sheria au sera yoyote dhidi yake, anaweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu kwa hati maalumu ya maombi kwa mujibu wa sheria za nchi ili kupata nafuu inayohitajika.

**(3)** Mahakama inaweza, kwa mujibu wa ibara ndogo ya (1), kutoa maelekezo itakayoona yanafaa, kuweka zuio, katazo au kuamuru jambo lifanyike ambalo lilikuwa limezuiwa.

**(4)** Shauri katika Mahakama la kudai haki za kikatiba kwa mujibu wa masharti ya Ibara hii laweza kufunguliwa na:
- **(a)** Mwanasheria Mkuu;
- **(b)** mtu anayejiwakilisha mwenyewe au taasisi inayowawakilisha wanachama wake;
- **(c)** mtu anayemwakilisha mtu ambaye hawezi kujiwakilisha mwenyewe kwa mujibu wa sheria za nchi; au
- **(d)** mtu anayewakilisha kundi la watu wenye malengo yanayofanana au jamii ya watu fulani ambao haki zao zimevunjwa.

**(5)** Endapo katika shauri lolote inadaiwa kwamba sheria yoyote iliyotungwa au hatua yoyote iliyochukuliwa na Serikali au mamlaka nyingine inafuta au inakataza haki, uhuru na wajibu muhimu utakaotokana na Ibara ya 31 hadi 56 za Katiba hii, na Mahakama Kuu kama inaridhika basi itatoa tamko kwamba sheria au hatua ina-yohusika ni batili au kinyume cha Katiba.

**(6)** Iwapo Mahakama Kuu itaona kuwa inafaa, hali au maslahi ya jamii yanahitaji hivyo, badala ya kutamka kuwa sheria au hatua hiyo ni batili, Mahakama Kuu itakuwa na uwezo wa kuamua au kutoa fursa kwa mamlaka nyingine yoyote inayohusika kurekebisha hitilafu iliyopo katika sheria au hatua inayolalamikiwa ndani ya muda utakaopangwa na Mahakama hiyo, sheria au hatua hiyo itaendelea kuwa ni halali hadi ma-rekebisho yatakapofanywa au muda uliowekwa na utakapokwisha, ili mradi muda mfupi zaidi ndio uzingatiwe.

**Kwa ibara hii ni kwamba haki zilizoanishwa katika sura hii ya haki za binadamu zinaweza  kudaiwa mahakamani pale ambapo mtu atapokonywa haki yake.**

| | | |
|---|---|---|
| **SURA YA 6: URAIA KATIKA JMT** | **Ibara 70(1):** Kila mtu aliyezaliwa Tanzania Bara au Zanzaibar atakuwa raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano iwapo, wakati wa kuzaliwa, mama au baba yake ni, au alikuwa raia wa Jamhuri ya Muungano **(2)** Kwa mujibu wa masharti ya katiba hii, mtu aliyezaliwa nje ya Tanzania atakuwa ni raia wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania wa kuzaliwa kuanzia tarahe ya kuzaliwa kwake ikiwa mama au baba yake ni raia wa JMT **(3)** Endapo mmoja kati ya wazazi wake alifariki kaba ya mtu huyo kuzaliwa, uraia wa mzazi huyo wakati wa kifo chake utatumika kwa madhumuni ya kutambua uraia wa mtu huyo aliyezaliwa baada ya mzazi aliyefariki kana kwamba mzazi huyo alikuwa anaishi hadi kuzaliwa kwa mtu huyo | Kwa mara ya kwanza wanawake wa nchi hii wamepewa haki sawa za uraia ikiwa ni pamoja na haki ya kurithisha watoto wao uraia. |
| **SURA YA 7,8 & 9: MUUNDO , UHUSIANO & URATIBU WA MAMBO YA JMT** | Kimsingi, kwenye hili la muundo, uhusiano na utaratibu wa mambo ys JMT, Mtandao wa Wanawake na Katiba ulitoa msimamo kuwa mfumo wa serikali utakaopendekezwa usiwabebeshe mzigo wanawake na wanaume maskini zaidi. Ila ni muhimu mfumo huo uweke utaratibu wa uwajibikaji kwa wananchi, wakiwemo wanawake kwa wanaume. | |
| **SURA YA 10: BUNGE LA JMT** | **Ibara ya 129(4)** Msingi wa uwakilishi katika uchaguzi wa wabunge utazingatia uwakilishi ulio sawa kati ya wabunge wanawake na wanaume. | Msingi wa kikatiba unaolenga katika uwakilishi ulio sawa kijinsia ni ushindi mkubwa kwani unatoa nafasi kwa wanawake zaidi -wagombea- katika Bunge na hivyo kuimarisha misingi ya usawa wa jin-sia katika uongozi nchini. Msingi huu utawajibisha vyama vya siasa kusimamisha wagombea wenye sifa, na kuwawezesha wagombea wao wanawake na wanaume kushinda kwenye majimbo yao |
| **SURA YA 13: UTUMISHI WA UMMA KATIKA JMT** | **Ibara 208(1)** Kutakuwa na utumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utakaozingatia misingi mikuu ifuatayo: **(c)** Kuhakikisha kwamba uteuzi na ajira katika nafasi mbalimbali unazingatia uwezo wa kitaaluma, weledi, maarifa, ujuzi, usawa wa kijinsia na uzoefu katika eneo husika na fursa kwa watu wenye ulemavu | Ibara hizi katika Katiba Pendekezwa, zinaondosha dhana hapo juu kwamba usawa wa jinsia haukuzingatiwa Ibara hii imezingatia (Bunge litatunga sheria kuhusu hili). |
| | **Ibara 209 (2)** Bila kuathiri masharti ya ibara ndogo ya **(1)**, uteuzi wa kiongozi na mtumishi katika taasisi au wizara ya Muungano utafanyika kwa kuzingatia uwakilishi wa pande mbili za Muungano, usawa wa jinsia na watu wenye ulemavu | Katiba Pendekezwa imezingatia misingi ya **usawa wa jinsia** kwa watu wenye ulemavu katika kuteuliwa kushika nafasi katika taasisi au Wizara za Muungano.<br><br>Hii inawajibisha pande mbili za muungano kuzingatia masharti haya ya kiKatiba. |

| | | |
|---|---|---|
| | | Hili ni jambo ambalo limekuwa likipiganiwa kwa miaka mingi na kipengele hiki kinatosha kuziba viraka katika maeneo yote ya uteuzi wa nafasi mbalimbali kama zilivyoainishwa katika Katiba Pendekezwa hii.<br><br>**Kipengele hiki ni cha kimapinduzi na ni ukombozi mkubwa kwa wanawake na makundi ambayo yalikuwa hayapati haki stahiki za kushika nyadhifa mbalimbali.** |
| **SURA YA 14: UCHAGUZI KTK VYOMBO VYA UWAKILISHI & VYAMA VYA SIASA** | **Ibara ya 216(1):** Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 88 na 140, mtu atakuwa na haki ya kuwa mgombea huru katika uchaguzi unaosimamiwa na ume Huru ya Uchaguzi | Kwa mara ya kwanza Katiba Pendekezwa imetambua haki za MGOMBEA HURU bila kupitia chama chochote cha siasa ila masharti yaliyowekwa yanaweza kuwa kikwazo. |
| | **Ibara ya 224 (2):** haitakuwa halali kwa chama chochote cha siasa kusajiliwa ambacho kutokana na katiba au sera yake **(e)** hakiruhusu uongozi wake kuchaguliwa kwa kuzingatia jinsi, watu wenye ulemavu na wakilishi wa pande zote mbili za Muungano kwa njia ya kidemokrasia | Kwa mara ya kwanza katika historia ya maendeleo ya kisiasa ya Tanzania, vyama vya siasa wanawajibishwa kuzingatia usawa wa kijinsia katika nafasi za uongozi kama sharti la usajili. Inafahamika wazi kuwa vyama vya siasa ndio vinasimamia nani aingia katika siasa na kwa wadhifa gani. Ikiwa ibara hii katika Katiba Mpya itaheshimika, kwa uhakika itabadilisha hali iliyoko hivi sasa ambapo vyama vyote vya siasa vimekuwa vikionyesha dalili za mfumo dume katika uongozi. Hii ni pamoja na kuwa wanawake wengi wametumika sana katika uhamasishaji, vyama vyao vimewaacha kabisa katika uongozi nchini. |
| **SURA YA 15: TAASISI ZA UWAJIBIKAJI** | **Ibara ya 238 (1):** kazi na majukumu ya Tume yatakuwa kama ifuatavyo: **(b)** Kuhamasisha, kulinda na kufuatilia utekelezaji wa usawa wa jinsia na ulinganifu kwa ujumla katika maendeleo ya Taifa; **(c)** kupokea malalamiko juu ya uvunjaji wa haki za binadamu kwa ujumla | Katiba pendekezwa inatoa uwajibikaji kati-ka ufuatiliaji wa utekelezaji wa misingi ya Katiba. Ingawa pendekezo la kuwepo kwa Tume mahususi ya kusimamia usawa wa kijinsia halikupokelwa, bado Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora imepewa kama mojawapo ya kazi yake jukumu la kusimamia ufuatiliaji wa utekelezwaji na wa usawa wa kijinsia<br><br>Hili ni **FANIKIO** kubwa kwa wanawake nchini kwa kuwa suala la uwajibikaji na usimamizi wa ufuatiliaji wa utekelezaji wa haki za wanawake nchini. |

| | | |
|---|---|---|
| **SURA YA 16: MASHARTI KUHUSU FEDHA ZA JMT** | **Ibara ya 250:** Misingi katika Ibara hii itaongoza matumizi ya fedha za umma katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **(d)** taarifa za usimamizi wa fedha za umma zitatolwa katika lugha inayoeleweka kwa wananchi | Kwa wanawake nchini, hili lilikuwa ni dai la muda mrefu kwamba wananchi waweze kupata taarifa kuhusu masuala ya matumizi ya fedha kwa lugha rafiki. Msingi huu katika Katiba Pendekezwa utatoa nafasi ya kuwajibisha vyombo vya serikali kuandaa bajeti zinazozingatia usawa wa jinsia kwa ufanisi zaidi. |

# HITIMISHO

Harakati za kutetea haki za binadamu na hususani za wanawake na watoto zilitumia mwanya uliojitokeza kwa kupitia mchakato wa Katiba Mpya. Kwa kupitia mkakati wa ujenzi wa nguvu za pamoja za Mitandao, mbalimbali, ukiwemo Mtandao wa Wanawake na Katiba Tanzania, wanamtandao walishriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za Mchakato huo wakiwa na NIA ya kuhakikisha Katiba mpya inakitisha masuala ya usawa wa jinsia katika Sheria Mama ya nchi. Juhudi hizi zimepelekea kupatikana kwa Katiba Pendekezwa ambayo, pamoja na mapungufu yaliyopo, imejenga misingi au mihimili ya kikatiba itakayotoa fursa na mwanya wa kupatikana kwa Katiba Mpya yenye mrengo wa kijinsia. Jedwali hili limetoa vielelezo vya jinsi misingi inayopelekea katika kukuza katika Ibara mbalimbali za Katiba hii Pendekezwa.

Mtandao wa Wanawake na Katiba Tanzania, unatambua mapungufu yaliyojitokeza kwenye Katiba Pendekezwa, yakiwemo yale yanayondoa haki wananchi, wanawake kwa wanaume, ya kuwawajibisha viongozi au wabunge wao;  kutokuwepo kwa msimamo wa pamoja kuhusu mfumo na muundo wa serikali na mengineyo.



**Mtandao huu unaratibiwa na:**

Women Fund Tanzania
659 Mikoroshini Street
P.O.Box 79235 Dar es Salaam
Mob: +255 753 912 130
Email: info@wft.or.tz
www.wft.or.tz

MTANDAO WA WANAWAKE NA KATIBA

WOMEN FUND TANZANIA